# MAPITIO YA MWENENDO WA SOKO KWA WIKI 11APRIL 2025

**KARIBUNI TENA KATIKA KIPINDI CHETU CHA KILA WIKI KINACHOKUHABARISHA KUHUSU MWENENDO WA SOKO LA HISA LA DAR-ES-SALAAM, NA KULETWA KWENU NA VERTEX INTERNATIONAL SECURITIES, PAMOJA NANYI LEO NI MIMI,**

Kwa wiki inayoishia tarehe 11 April 2025, mauzo katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) yalipungua kwa asilimia 63.24 kutoka TZS 13.09 bilioni hadi TZS 4.8 bilioni. Kiasi cha hisa zilizouzwa kilipungua pia kwa asilimia 42.45 kutoka hisa milioni 4.1 hadi hisa milioni 2.37.

Jumla ya Mtaji wa Soko ulipungua kwa asilimia 0.77 kutoka TZS 19.21 trilioni hadi TZS 19 trilioni.Hii nikutokana na kupungua kwa bei ya hisa za JHL,EABL,NICOL,NMG na MKCB,ambapo JHL ilipungua bei kwa asilimia 4.18 , EABL ikipingua bei kwa asilimia 2.89, NICOL ikipingua bei kwa asilimia 1.39, NMG ikipingua bei kwa asilimia 3.57 na MKCB ikipingua bei kwa asilimia 6.9. Mtaji wa Soko la Ndani uliongezeka kwa asilimia 0.1, kutoka TZS 12.96 trilioni hadi TZS 12.98 trilioni kutokana na kuongezeka kwa bei ya hisa za TPCC ambazo ziliongezeka kwa TZS 80 na AFRIPRISE ambazo ziliongezeka kwa TZS 10.

CRDB iliongoza kwa idadi kubwa ya hisa zilizouzwa kwa asilimia 67.78 sawa na hisa milioni 1.6 ikifuatiwa na TBL kwa asilimia 18.21 sawa na hisa 432,313 na TPCC ikiwa ni asilimia 3.46 sawa na hisa 82,018.

TBL imeongoza kwa mauzo ya hisa wiki hii ikirekodi TZS 2.8 bilioni, ambayo ni 59.84% ya mauzo yote ikifuatiwa na CRDB Ikirekodi TZS 1.26 billion ambayo ni asilimia 26.34, huku TPCC ikirekodi 329M ambayo ni sawa na asilimia 6.86 ya mauzo yote.

Wawekezaji wa ndani wamechangia asilimia 99.94 huku wawekezaji wa kigeni wakichangia asilimia 0.06 tu kwenye shughuli za soko wiki hii.

Katika wiki kulikuwa na miamala 150 kwenye soko la hatifungani, ambapo soko lilisajili takribani TZS 139.5 bilioni.

Mnada wa dhamana za Serikali za muda mfupi (Treasuty bill ) wa siku 35 na siku 364 uliofanywa na Benki Kuu ya Tanzania tarehe 09 April 2025, ulisajili zabuni 2 kwa mnada wa siku 35 na zabuni 38 kwa mnada wa siku 364 ambapo zabuni zote zilifanikiwa na kukusanya kiasi cha TZS 137.7 Bilioni.

**MPAKA HAPO TUMEFIKIA MWISHO WA MAPITIO YA SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM KWA WIKI ILIYOISHIA IJUMAA YA APRIL 11, 2025. KWASASA UNAWEZA KUPATA HUDUMA ZETU KUPITIA MATAWI YA SHIRIKA LA POSTA YALIYOPO NCHI NZIMA .#TUMEKUFIKIA WEKEZA CHAP CHAP. MPAKA WAKATI MWINGINE MIMI NI**